# Kiwanda cha nyama Nguru kuwanufaisha wafugaji

Na Thadei Hafigwa

NI mageuzi makubwa ya kifikra yamefanywa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), kwa kufanya uwekezaji mkubwa katika sekta ya mifugo, ambapo umejenga Kiwanda cha Kuchakata Nyama kwenye Ranchi ya Nguru Hills kwa kiwango cha kimataifa. Kiwanda hicho kipo Wilaya ya Mvomero mkoani Morogoro.

Kwa sasa eneo la Nguru lililopo kilometa chache kutoka mjini Morogoro limepata umaarufu ndani na nje ya nchi kutokana na uwepo wa kiwanda hicho chenye mitambo na teknolojia ya kisasa cha kuchakata nyama katika kiwango cha juu na kuongeza thamani ya bidhaa hiyo inayochangia pato la Taifa na kutoa ajira.

Miaka ya nyuma jamii ya wakulima na wafugaji wilayani Mvomero walijikuta wakiingia kwenye sintofahamu kwa kuwepo migogoro ya mara kwa mara kutokana na mifugo kula mazao ya wakulima.

Miongoni mwa sababu zinazotajwa na kusababisha kutokea kwa hali hiyo, ni ufugaji wa kimazoea, kuongezeka kwa idadi kubwa ya mifugo iliyopo wilayanini humo lakini kwa sasa hali itabadilika kwani mifugo itakuwa inauzwa kwenye kiwanda hicho ambapo wananenepeshwa ndani ya ranchi kabla ya kuchinjwa.

Kimsingi jitihada za kukabiliana na hali hiyo zimefanywa huku PSSSF ikitumia changamoto hiyo kuwa fursa ya uwekezaji wa kiwanda cha kuchakata nyama na hivyo kuwa muarobaini kwa tatizo hilo.

Aidha, PSSSF baada ya kufanya utafiti ilibaini kuwa wilaya hiyo ina mifugo mingi, hivyo inaweza kufanya uwekezaji wa kiwanda cha kuchakata nyama ili kukidhi soko la kitaifa na kimataifa na kuleta tija katika maendeleo ya sekta ya mifugo nchini.

Hivi karibuni wanachama wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), baada ya mkutano wao wa kitaaluma uliofanyika mjini Morogoro kwa siku tatu walitembelea Kiwanda cha Nyama kilichopo Ranchi ya Nguru Hills na kujionea uwekezaji mkubwa uliofanywa na PSSSF na kuelezwa kuwa kiwanda hicho kwa siku kinachinja mbuzi 1,000 na ng'ombe 100.

Meneja wa Kiwanda cha Nguru Hill, Eric Cormack alisema kuwa asilimia 80 ya mauzo inakwenda nje ya nchi huku asilimia 20 zikiuzwa nchini, hivyo kuchagiza ongezeko la uchumi kwa wakazi wa Morogoro na Taifa kwa ujumla.

Alisema kuwa soko kubwa la bidhaa za nyama inayochakatwa katika kiwanda hicho lipo nchi za Uarabuni, China, Vietnam, Kuwait, Qatar, Umoja wa Falme za Kiarabu (Dubai) na kwamba Saudi Arabia pekee hitaji lao la nyama kwa mwaka ni tani 700,000.



Nyama ya ng'ombe ikiwa katika uchakataji.

*"Mara kadhaa tumekuwa tukishuhudia uwekezaji kama huu katika maeneo mbalimbali, lakini baada ya muda mfupi unaanza kulegalega kutokana na kukosekana kwa uaminifu na utunzaji na hivyo kubaki historia, tusikubali kuharibu uwekezaji huu, wafanyakazi msiwe na tabia ya udokozi na wizi," alisema.*

Akieleza utaratibu wa kiwanda hicho katika kununua mifugo, meneja huyo alisema kuwa ng'ombe anatakiwa awe na umri usiopungua miaka mitano na kuwa na uzito usiopungua kilo 215 ili baada ya kunenepeshwa aweze kufikia kilo 390.

Kwa hapa nchini hususan wakazi wa Dar es Salaam na mikoa mingine wanaweza kununua nyama na kuipata popote walipo ambapo wanasafirishiwa hadi walipo.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile alisema kuwa viwanda vya aina ya Nguru Hill ni vingi katika nchi zilizoendelea hakuna mtu anaweza kuchinja ng'ombe au mbuzi nyumbani kwake, ambapo jamii ikibadili mtazamo kwa kuacha mfumo wa kizamani na kufuata njia ya kisasa kutakuwa na uhakika wa kula nyama katika viwango vyenye ubora na wa kimataifa.

"Katika kiwanda hiki cha kuchakata nyama cha Nguru, Wahariri tumeshuhudia kuanzia geti la kuingilia eneo la kiwanda kumewekwa utaratibu wa kudhibiti magonjwa kutoingia kiwandani kumewekwa maji yenye dawa, kabla ya kutembelea kiwanda kila mmoja amepewa vazi maalumu, kuanzia unyayoni (viatu), kofia maalumu na barakoa ili kudhibiti magonjwa kuingia kiwandani," alieleza.

Aidha, Balile ameshauri uongozi wa PSSSF kutunza uwekezaji huo kwa maslahi mapana ya nchi na kuwasihi wafanyakazi kuwa waaminifu na waadilifu katika kazi zao.

"Mara kadhaa tumekuwa tukishuhudia uwekezaji kama huu katika maeneo mbalimbali, lakini baada ya muda mfupi unaanza kulegalega kutokana na kukosekana kwa uaminifu na utunzaji na hivyo kubaki historia, tusikubali kuharibu uwekezaji huu, wafanyakazi msiwe na tabia ya udokozi na wizi," alisema.

Balile alitumia fursa hiyo kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan kwa maono aliyokuwa nayo ya kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji kutoka sekta binafsi kushirikiana na serikali katika kuleta mabadiliko ya kiuchumi nchini.

Kwa upande wake, Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma wa PSSSF, James Mlowe alieleza kuwa Mkoa wa Morogoro ni miongoni mwa mikoa yenye mifugo mingi, ambapo siku za nyuma kulikuwa na matukio ya migogoro ya mara kwa mara kati ya wakulima na wafugaji katika Wilaya ya Mvomero.

Mlowe alisema uwepo wa machinjio ya kisasa katika kawanda cha Nguru Hill umetoa suluhisho la soko la uhakika na wafugaji kuboresha maisha yao kutokana na kupata pato kubwa baada ya kuuza mifugo yao hapa kiwandani kwa bei nzuri.

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Dk. Rose Reuben ambaye pia ni mwanachama wa Jukwaa la Wahariri alisema kuwa teknolojia inayotumiwa katika kiwanda hicho kuanzia machinjio, uchunwaji wa ngozi na vifungashio vya nyama katika ujazo tofauti kulingana na hitaji la mteja umezingatia viwango vya kimataifa.

Alisema kuwa hata mfumo wa ajira uliopo katika kiwanda hicho umezingatia jinsia ambapo kuna wafanyakazi wa kiume na wakike. Alisema jambo hilo limemvutia na kuipongeza menejimenti ya kiwanda kwa kutoa ajira bila ya upendeleo.

CamScanner

• Kampuni 20 zapata vibali gesi ya magari NDANI

ISSN 1821-570X
TOLEO NA. 05681
JUMATANO
APRILI 12, 2023
TSH. 1,000
KSH. 100
www.habarileo.co.tz

uk 2.

# HabariLEO

GWIJI LA HABARI TANZANIA

@Habarileo Habarileo dailynews_habarileo dailynews_habarileo




NDANI

## WANACHAMA 468 NHIF WAFUNGIWA KWA UDANGANYIFU

uk3

## UMMY AITA WAWEKEZAJI MIFUKO YA DAMU

uk7

## TAASISI YATAJA VIGEZO VIJANA KULIPIWA MAHARI

uk4

# Benki ya Dunia yasifu usimamizi uchumi

uk3



Makamu wa Rais, Dk Philip Mpango akisikiliza maelezo kutoka kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (kushoto) wakati akikagua maendeleo ya Shamba la Mifugo Mabuki mkoani Mwanza jana baada ya Serikali ya Awamu ya Sita kupeleka ng'ombe aina ya mitamba 500 katika shamba hilo. (Picha na Ofisi ya Makamu wa Rais).

## Mpango: Mifugo ipewe umuhimu dira 2025-2050

uk2

• Vituo vinane kufundisha vijana kufuga kibiashara

## DK MWINYI AKUTANA NA TUME YA MABORESHO YA HAKI JINAI

uk7

## VYAKULA VYAPUNGUZA MFUMUKO WA BEI

uk7

## LATRA YAFUNGIA MABASI 27, LESENI ZA MADEREVA ZASITISHWA

uk4

CamScanner

HABARILEO JUMATANO APRILI 12, 2023

HABARI LEO UK 2.

# Mpango: Mifugo ipewe umuhimu dira 2025-2050

Na Abela Msikula

MAKAMU wa Rais, Dk Philip Mpango amesema ni muhimu Dira mpya ya Maendeleo 2025-2050 itoe umuhimu kwa pekee kwa sekta ya mifugo ili taifa linufaishwe na wingi wa mifugo kwa kufuga kibiashara.

Amepongeza msukumo wa Rais Samia Suluhu Hassan uliowezesha Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuanzisha vituo vinane vya kutoa mafunzo kwa vijana wafuge kibiashara.

Dk Mpango ameyasema hayo mkoani Mwanza jana alipotembelea Kituo Atamizi cha Shamba la Mifugo la Mabuki likiwa ni mojawapo ya mashamba matatu yaliyoanza kutoa mafunzo kwa vijana 240 ili wafuge kibiashara.

Alisema vituo hivyo ni mkombozi wa sekta ya mifugo nchini kwa kuwa mifugo itanenepeshwa na kubadilishwa ili kuiongezea thamani.

"Kama ni kwenda na mimi kupiga magoti kumwomba Mheshimiwa Rais viongezeke nitafanya hata leo…yaani ninyi kweli ndio mfano katika taifa hili katika kubadilisha sekta yetu ya mifugo.

"Tuache kuimba tu tuna ng'ombe wengi, tuna mbuzi wengi halafu vijana wetu wanalia hawana kazi, hawana kipato mfukoni, kwa hiyo hapa dawa imepatikana, tutalisimamia hili kikamilifu," alisema Dk Mpango.

Aliongeza: "Mimi nawahesabu ninyi ndio waanzilishi kubadilisha kabisa mifugo ya taifa hili itupatie chakula, nyama, maziwa, itupatie kipato, itupatie ajira. Hii mambo ya wewe umesomea mifugo halafu unarudi unasema sina kazi, sasa hapa ndio mkombozi wake."

Alisema kuanzishwa kwa vituo hivyo ni hatua kubwa na kwamba sasa Tanzania itaanza kupata mabadiliko ya kweli kwenye sekta ya mifugo.

Alisema atashawishi Wizara ya Mifugo na Uvuvi iongezewe bajeti ili kuendeleza mafunzo hayo kwa vijana, na pia atamwomba Rais Samia vituo hivyo vipatiwe umeme wa uhakika na mashine za kuchakata vyakula vya mifugo.

"Haiwezi kuwa sisi tunajidai katika Afrika tunasema ndio taifa lenye mifugo mingi, taifa la tatu kwa mifugo katika Bara la Afrika lakini mauzo yetu ya nyama huko nje bure," alisema Makamu wa Rais.

Alisema aliwaeleza Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) mkoani Morogoro kwamba hapendi utaratibu wa vijana kusoma kilimo, kuwa na walimu na wakufunzi wa kilimo, lakini wao hawafanyi shughuli hizo.

"Maprofesa wanafundisha kilimo, lakini wao wenyewe hawapo wanakwenda kujenga gesti house (nyumba za kulala wageni). Wanakwenda kutengeneza hoteli, humuoni mtaalamu aliyesomea kilimo akitekeleza shughuli za kilimo," alisema Dk Mpango.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega alisema kila mwaka vijana 1,600 wanahitimu mafunzo ya astashahada, stashahada na shahada kwenye mifugo, lakini 150 tu kati yao huingia kwenye mfumo rasmi wa sekta hiyo.

Dk Mpango alielezwa kuwa katika mwaka huu wa fedha, wizara hiyo imepanga kununua ng'ombe 2,400 kwa ajili ya mafunzo ya ufugaji kibiashara, lakini hadi sasa wamenunuliwa 2,150 wenye kilogramu kuanzia 150 wenye umri kuanzia miaka miwili hadi minne.

CamScanner

wa bia aina ya Pilsner wanaof

UVUVI - MWANANCHI UK 9

# Sekta ya uvuvi yakabiliwa na changamoto

Jesse Mikofu, Mwananchi
jmikofu@mwananchi.co.tz

**Unguja.** Licha ya uvuvi na ukuzaji wa viumbe kwenye maji kuwa na mchango mkubwa katika sera ya uchumi wa bluu, kuna changamoto za mbegu na chakula zinazosababishwa na mabadiliko ya tabianchi, imeelezwa.

Kutokana na changamoto hiyo, umezinduliwa mradi wa utafiti wa bahari, mazingira na maliasili uliobuniwa na Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (Suza) kwa udhamini wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (Costech).



"Natoa wito kituo kifanye tafiti zenye tija kwa wananchi na kuleta suluhisho la matatizo yanayowakabili sambamba na kutoa mafunzo kwa wavuvi na vijana wanaosomea fani hiyo hapa nchini."

Suleiman

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mkuu wa Kituo cha Utafiti Suza, Dk Mary Mtumwa Khatib alisema mradi utapunguza changamoto hizo kwa kutumia tasnia ya utafiti kwa ujenzi wa miundombinu ya utafiti, maabara ya ubora wa maji na chakula cha samaki.

"Miundombinu hii ina uwezo wa kufanya tafiti na kuhaulisha teknolojia ya uzalishaji wa vifaranga vya aina mbalimbali ya viumbe vya baharini," alisema Dk Mary.

Mkurugenzi Mkuu wa Costech, Dk Amos Nungu alisema miaka minne iliyopita Costech imetoa Sh1.7 bilioni kugharamia shughuli za utafiti na ubunifu Zanzibar.

Pia, alisema inaendelea kutekeleza mkakati wa kuhakikisha bunifu hizo zinapata usimamizi wa kutosha na mwaka wa fedha uliopita ilitoa Sh150 milioni kuhakikisha kuwapo na ukumbi mama wa kuratibu shughuli za ubunifu.

Kwa kuzingatia dira ya kukuza uchumi wa bluu Zanzibar, mwaka 2021 tume iliidhinisha Sh400 milioni ili kuboresha miundombinu ya utafiti kwenye sekta ya uchumi wa bluu.

"Tunategemea itakuwa ni kichocheo katika kaulimbiu ya Serikali kuhusu uchumi wa bluu," alisema.

Makamu Mkuu Suza, Profesa Moh'd Makame alisema mradi huo utakusanya wataalamu kutoka maeneo mbalimbali kufanya tafiti zitakazoleta maendeleo makubwa kupitia sera ya uchumi wa bluu.

Akifungua mradi huo, Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla alisema kumekuwapo na tatizo sugu la kufanya tafiti, lakini matokeo yake huishia kwenye makaratasi na maabara bila kutumika.

Suleiman alisema tafiti za namna hiyo huitia hasara Serikali na hazileti tija kwa wananchi, hivyo kutaka kituo hicho kifanye tafiti zitakazoleta tija.